


# Nafasi ya Kanisa kwa Umma

Jarida la Mafunzo la Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani

FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI

# Nafasi ya Kanisa kwa Umma

**Jarida la Mafunzo la Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani**

© Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, 2016

Mhariri: Idara ya Theologia na Ushuhuda kwa Umma

Usanifu na Mpangilio: Idara ya Theologia na Ushuhuda kwa Umma
Ofisi ya Huduma ya Mawasiliano

Picha ya Kitabu: Wajumbe wa FMKD kwa COP20, uliohusisha vijana watetea haki za hali ya hewa kutoka maeneo yote ya FMKD, waliokutana na Bi. Christiana Figueres, Mkurugenzi wa Umoja wa Mataifa wa Mfumo wa Makubaliano Kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi (UNFCCC) huko Lima. Wakati wa mkesha wa mazungumzo na dini mbalimbali kwa ajili ya hali ya hewa, siku moja kabla ya kongamano, Figueres alipewa alama ya mshumaa wa kijani kutoka kwa wawakilishi wa dini mbalimbali. Aliuleta mshumaa huo wakati wa ufunguzi wa kongamano la COP20, na baadaye alisema kwenye akaunti yake ya Twitter, "Mshumaa wenu wa mkesha ulikuwa mimbara ya kulifungua kongamano la COP20 leo. Mwanga huu uangaze mapatano yake." Picha: FMKD/Sean Hawkey

ISBN 978-2-940459-45-2

# Yaliyomo


Dibaji ..... 5

*Martin Junge*

Utangulizi ..... 7

Mjadala wa kimataifa kuhusu mchango wa dini sehemu za umma ..... 7

Ushiriki wa Mungu na dunia kama msingi wa nafasi ya kanisa sehemu za umma ... 9

Lengo na muundo wa andiko hili ..... 11

Sehemu za Umma kama Mahali pa Haki kwa Wote ..... 13

Mahali pa haki kwa wote ..... 13

Sehemu za umma - uhalisia wake ..... 14

Mipaka inayobadilika ..... 15

Makanisa kama sehemu ya umma ..... 16

Maswali kuhusu nguvu ya umma ..... 17

Kuwa Kanisa katikati ya Umma—Mtazamo wa Kilutheri ..... 19

Tumeokolewa kwa Neema - Wito unaotokana na ubatizo wetu ..... 19

Tofauti kati ya milki ya kiroho na kidunia ..... 20

Changamoto ya namna ya kuendana na tofauti hizi ..... 22

Maswali kuhusu tofauti ya dola mbili ..... 24

Tabia za Ushiriki wa Kilutheri kwa Umma ..... 25

Ujasiri na uwazi: Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma katikaimani ..... 25

Ustahimilivu na uvumilivu:Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma katika matumaini ..... 26

Mshikamano na uwezeshaji: Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma katika upendo ..... 26

Maswali kuhusu tabia ya uhusika wa Kilutheri kwa Umma ..... 27

Njia Zinazotumika na Kanisa Kujihusha Sehemu za Umma ..... 29

Mifano ya kujihusisha na umma ..... 29

Mfano 1: Kujihusisha na wakimbizi ..... 29

Mfano 2: Ushiriki katika kutatua suala ubaguzi ..... 29

Mfano 3: Kupigania haki ya kijinsia ..... 30

Mfano 4: Ushiriki katika kutetea haki ya tabia nchi ..... 31

Mfano 5: Kushiriki mazungumzo kwa ajili ya mahusiano ya amani na dini zingine ..... 31

Vipimo vitatu vya ushiriki kwa umma ..... 32

Maswali kuhusu uhusika wa kanisa ..... 33

ABCDE ya Uhusika wa Kanisa sehemu za Umma ........................................ 35
Kutathmini masuala ya umma kwa njia shirikishi ........................................35
Kujenga uhusiano wenye kuaminiana........................................................35
Kupinga uonevu ........................................................................................35
Kugundua alama za matumaini ..................................................................36
Kuwezesha wahitaji ...................................................................................36

Nafasi ya Kanisa kwa Umma - Tamko la Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani..................................................................................................37
1. Walutheri wanakubali wito wa kushiriki katika masuala ya umma............. 37
2. Walutheri wanaahidi kuimarisha ushiriki wao kwa umma kama sehemu ya haki kwa wote ..........................................................................................38
3. Walutheri wanakubali wajibu na majukumu ya jumuiya za kidini .............38
4. Walutheri wanakaza tofauti kati ya utawala wa kidunia na kiroho ............39
5. Walutheri wanatambua kuwa maeneo ya umma ni ya kushirikiana na watu wote..........................................................................................................39
6. Walutheri wanayakubali madai ya haki za binadamu kama nyenzo muhimu ya kuwezesha upatikanaji wa haki na amani..............................................39
7. Walutheri wameahidi kushughulikia mambo matano katika ushiriki wao kwa umma: ......................................................................................................40

Kikosi kazi cha kitaaluma ................................................................... 41
Wajumbe.................................................................................................. 41
Wafanyakazi wa FMKD ............................................................................... 41

# Dibaji

*Martin Junge*

"Tumeokolewa kwa neema ya Mungu" - tunakubali na kusherehekea ushiriki wa upaji wa maisha na furaha kuelekea jubile ya Matengenezo ya Kanisa ya 2017. Matokeo ya ushiriki huu unaenda mbali zaidi ya kuta za kanisa; ina matokeo yanayoonekana kwa umma. Matengenezo yalikuwa chachu ya mabadiliko, kwa kanisa na jamii kwa ujumla. Mashaka wa Martin Luther kuhusu uchungaji na huduma za diakonia ulimfanya auendee umma - kupinga, kukosoa na kushauri kwa misingi ya yale aliyoyaona kama kweli ya injili. Aliumia kwa sababu ya watu walioteseka, na ilitokana na hasira yake ya kinabii dhidi ya watu wenye nguvu ndani ya kanisa na jamii iliyomsukuma kuweka mbele ya maono yake ya kitheologia, yaliyojengwa katika sala na utafiti wa kitaaluma.

"Tumeokolewa kwa neema ya Mungu" - makanisa hujenga ushirika na kushiriki kwa vitendo ndani ya umma na kufanya kazi kutetea haki, amani na upatanisho. Wakati fulani hili linatokea katikati ya shughuli zinazoonekana, na wakati mwingine kanisa linashuhudia kwa sauti kubwa kwa njia ya huduma kwa majirani wenye uhitaji, kwa njia ya huduma za kidiakonia zinazoendelea kimya kimya au kwa wazi. Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), kwa njia ya makanisa washirika, mipango, na miradi yake, limeshiriki kwa uzito unaostahili kufanya kazi katika asasi za jumuiya kwa ajili ya kukuza amani na haki na kushiriki utetezi wa haki za binadamu.

Wakati huo huo, FMKD limeshiriki katika tafakari za kitheologia zinazoweka bayana uelewa wetu wa kuwa kanisa lililo katikati ya umma wa leo. Kongamano la FMKD, lililoitwa "Mawazo ya Kimataifa kuhusu Matengenezo. Uhusiano kati ya Theologia, Siasa na Uchumi," lililofanyika Windhoek, Namibia, ndani ya Siku ya Matengenezo ya Kanisa 2015, lilitoa uchambuzi wa kina na mawazo yenye msisimuko kwa kuleta ufahamu wa kitheologia kuhusu masuala ambayo leo yana mjadala mkubwa

katika umma. Mbali na hayo, FMKD lilikaribisha, kwa njia ya mikutano ya mashauriano iliyofanyika Januari 2014 kule Muenster, Ujerumani, Mei 2014, Dar es Salaam, Tanzania na Septemba 2015, Hong Kong, China washirika wa kiekumene na dini zingine ili kwa pamoja waone namna ambavyo jumuiya za kidini zinaweza kuwa mchango muhimu wa namna ya kuuimarisha umma.

Jaridahili la mafunzo liliandaliwa na kundi la kimataifa la Watheologia wa Kilutheri lililoteuliwa na Mkutano wa Maofisa wa FMKD mnamo Novemba 2014: Askofu Mkuu Dk. Antje Jackelén (Swedeni) kama Mwenyekiti, Askofu Mstaafu, Dk. Suneel Bhanu Busi (India), Mchg. Dk. Eva Harasta (Austria), Dk Eneida Jacobsen (Brazil), Kathryn Lohre (Marekani), Dk Jerzy Sojka (Poland). Kutokana na kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Kupambana na Umaskini na Ustawi wa Jamii wa Namibia, Askofu Mstaafu Zephania Kameeta aliacha na nafasi yake kuchukuliwa na Mchg. Lusungu Mbilinyi (Tanzania). Kikosi hiki cha kitaaluma kilikutana huko Evangelische Akademie Bad Boll, Ujerumani Januari 2015. Baadaye kikosi kilifanya kongamano Windhoek, Namibia Oktoba 2015. Na mwisho walifanya kongamano lingine Sigtuna Stiftelsen, Sweden Februari 2016. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wote wa kikosi hiki kwa kujitolea kwao bila kuchoka katika mchakato wa kuandaa mtaala huu.

Katika mkutano wa Wittenberg uliofanyika Juni 2016, Halmashauri Kuu ya FMKD lilipokea rasimu ya mtaala huu na kuupitisha kwa ajili ya matumizi ya makanisa wanachama kwa ajili ya mafundisho na utekelezaji. Nawaalika makanisa wanachama, vitengo vya programu na miradi, vyuo vya theologia, washirika wa kiekumene na dini zingine kuusoma mtaala huu na kujishughulisha na maswali yanayoibuliwa katika mtaala huu. Andiko hili ni rejea muhimu kwa ajili ya matukio ya kumbukumbu ya matengenezo ya kanisa na baadaye. Mtaala huu uwe nyenzo ya kuiwezesha jumuiya ya Kilutheri na washirika wake kujishughulisha kwa vitendo na masuala yaliyo ndani ya umma katika maeneo yao na kimataifa, ili pawe mahali pa haki kwa wote.

# Utangulizi

## Mjadala wa kimataifa kuhusu mchango wa dini sehemu za umma

Katika siku za karibuni, swali la zamani lililoulizwa na mwanadamu kuhusu mchango wa dini katika jamii, limepata msukumo kwa upya ndani ya umma. Kwa kuwa dini inagusa mioyo ya watu, akili na matendo, ina nguvu na ushawishi wa ajabu. Kuna mambo yaliyowazi yanayoonesha jinsi mawazo na matendo ya kidini yalivyochangia katika kukuza ustawi wa mtu kwa kuulinda utu wa watu na kutatua na kuukabili umaskini na mateso. Ulimwenguni kote, watu husimulia habari kuhusu jinsi imani yao au dini vina uwezo wa kulinda, kukomboa, kufariji, kuwezesha kubadili au kuponya maisha yao, kwa mtu mmoja mmoja au jumuiya kwa ujumla. Kwa sababu ya nguvu yake, dini imesifiwa na kushangiliwa, lakini wakati mwingine pia imetazamwa kwa woga na mashaka. Watendaji wa dini waliotenda kwa kudanganya, kukandamiza au njia za kikatili wamekuwa wakikosolewa na wakati mwingine kupingwa. Kokote kule ambako watendaji wa kidini wamekuwa na ushindani wa vyeo wao kwa wao, wameleta madhara ya uharibifu na migawanyiko na mashaka makubwa.

Kwa kuwa imani na kuwa mshiriki wa dini fulani kunawapa watu nguvu na kuwawezesha, inaweza pia ikasababisha hali hatarishi. Dini wakati mwingine inazidisha nguvu ya mamlaka, lakini pia ina uwezo wa kuonesha na kufunua nguvu za mamlaka zilizofichika, uonevu na hali hatarishi.

Swali kuhusu mchango wa dini katika jamii linagusa hali nzima ya uzoefu wa watu katika maisha, lakini pia kuibua hali ya mashaka ya kimifumo. Pamoja na dini kuwa au kutokuwa suala la umma au la mtu binafsi na jinsi anga za kidunia au kidini zinavyotakiwa kutofautishwa katika jamii bado limekuwa kwenye mjadala mkubwa. Kimataifa, mjadala huu unashawishiwa na mada kubwa angalau tano:

- **Dini na siasa:** Ni jinsi gani jumuiya za kidini, wanaharakati wa kisiasa na taasisi vinahusiana? Nini mifumo ya kikatiba na kisheria kwa ajili ya maisha ya kidini katika jamii na ni kwa jinsi gani watu wa imani wanayaishi maisha yao ya kiraia katika jamii zao? Ni jinsi gani wanaharakati wa kidini wanavikubali au kuvikandamiza viwango vya haki binadamu za kimataifa?

- **Dini na Uchumi:** Ni kwa jinsi gani watu wa dini wanasemea kwa ufasaha jinsi wanavyotarajia haki itendeke katika kijamii? Je watu wa dini wanafanya nini kama wazalishaji, walaji na wafanyabiashara katika muktadha mpya wa soko huria? Jumuiya za kidini zinaitikia vipi hali hii ya kuwa mantiki ya kisoko ndio imekuwa dhana iliyotawala katika kila eneo la maisha ya mtu?

- **Dini na Utamaduni**: Ni kwa jinsi gani jumuiya za kidini zinatoa majibu ya jinsi utamaduni unavyoathiri namna watu wanavyoelewa, tafsiri na kuchambua ukweli? Ni kwa jinsi gani jumuiya za dini zinatumia misemo ya kitamaduni, kama vile njia za mawasiliano, na ni jinsi gani mawasiliano yanaitumia dini? Je kuna udadisi au kujidadisi kuhusu matumizi mazuri au mabaya ya mawasiliano? Ni kwa jinsi gani aina mbalimbali za mawasiliano na njia nyingine za kujieleza kitamaduni zinasaidia kuzuia kujenga anga ya umma katika jamii?

- **Dini na Ukatili:** Ni kwa jinsi gani jamii za kidini zinakabiliana na ukatili majumbani, mitaani, na katika taasisi? Ni kwa namna gani mafundisho na matendo ya kidini yanaafikiana au kukaribisha vitendo vya kikatili, na yanaondoa ukatili na kusaidia upatanisho? Jumuiya za kidini zinaletaje maono ya amani sehemu za umma kwa njia zinazokubalika na zinazoonekana?

- **Dini na Sayansi:** Je kuna uhusiano wa mitazamo ya kidini na kisayansi? Ni ufahamu gani wa kisayansi unaweza kulisaidia kanisa kukuza ushiriki wake kwa umma? Je imani yetu katika sayansi na elimu imani (theologia na matendo ya kidini) vinaweza kufanya kazi pamoja kwa lengo zuri la pamoja katika dunia hii?

Katika nyakati ambapo katika nchi nyingi mijadala ya kisiasa imewagawa watu, ni muhimu kwamba jumuiya za kidini zishirikishe wanawake, wanaume, na vijana katika kuleta majibu ya maswali haya - pande zote, ndani na nje ya jumuiya - katika mazingira yanayotofautiana kama vile kwenye mikutano ya kiuongozi na kwenye mijadala katika vyuo vya theologia, mikutano ya jumuiya za kidini na katika mikusanyiko ya kiibada. Mada zote tano zinaathiri kwa mapana na kwa kina uwepo wa sehemu za umma katika jamii.

Jumuiya za kidini huweka kwa ufasaha namna masimulizi tofauti ya kiimani yanavyohamasisha ushiriki wa jumuiya hizo kwa umma wakati huo zikisikiliza na huku zikijua wazi tofauti ya mitazamo ya dhamira za kidini na zisizo za kidini. Katika mchakato huu, jumuiya zinatazama na kuthibitisha maeneo ya pamoja, na kwa njia ya mahusiano haya zinafikia muafaka wa kuheshimu tofauti zao.

## Ushiriki wa Mungu na dunia kama msingi wa nafasi ya kanisa sehemu za umma

Mungu anaupenda ulimwengu na hakomi kuhusika nao: dhamira hii ya ndani inahamasisha makanisa hushiriki katika sehemu za umma. Mungu aliumba dunia kwa njia ya Neno na akalipa uhai kwa njia ya Roho. Katika kufanyika mwili kwa Yesu Kristo, Mungu aliingia ndani ya dunia katika hali ya kipekee kabisa, akiwa na huruma ya ndani sana katika furaha na mateso, na matumaini na maumivu ya dunia hii. Ndani ya Yesu Kristo Mungu anasherehekea furaha ya ndoa kule Kana, akihakikisha kuwa mvinyo kwa watu wote unapatikana. Ndani ya Yesu Kristo, Mungu anavumilia mateso na kifo kilicho mdhalilisha msalabani, akihakikisha kuwa kila kona ya maisha ya mwanadamu, na hata yale mateso mengi ya kikatili na maumivu, vinabeba ahadi ya uwepo wa Mungu. Mungu alichagua kufanyika mwili ndani ya Yesu Kristo kama njia ya yeye kujifunua kwa wanadamu na uumbaji wote. Ushiriki wa Mungu katika dunia hii unaifanya theologia na matendo ya kanisa kuifikia duniani - katika sehemu za umma.

Kama makanisa na Wakristo tumeumbwa kwa njia ya ujumbe wa injili, nguvu iokoayo inayotubadilisha sisi tuishi maisha ambayo yanaakisi injili. Ugunduzi mpya wa kuhesabiwa haki kwa neema kwa njia ya imani uliofanywa na Matengenezo ya Kanisa unajumuisha maono mapya ya haki ndani ya jamii na watu waliobadilishwa, kanisa na taasisi nyinginezo. Uangavu wa kiroho unaotokana na uelewa wa kina wa ujumbe wa injili, umeiweka huru nguvu ya ajabu ili kuchangia mabadiliko katika jamii. Mfano halisi ni njia ya kimkakati ya kutatua tatizo la umaskini kwa njia ya taasisi ya mfuko wa pamoja na kwa hiyo kwa njia hiyo kufanya jumuiya kutimiza madai yake ya kutunza maskini. Wanamatengenezo waliwaambia watu wenye maamuzi ya kisiasa na nguzo zenye nguvu ya kiuchumi sio tu kupunguza umaskini kwa watu wenye uhitaji wa haraka, bali pia wapambane na sababu zinazosababisha umaskini, ukandamizaji wa kiuchumi na ujinga.

Elimu kwa wote, jambo lililokuwa kipaumbele cha Matengenezo ya Kanisa, imeendelea kuwa katika moyo wa uwepo wa kanisa kwa lengo la kuwawezesha watu kuwa vyombo vilivyokomaa katika kuboresha maisha yao na kuwa na mchango wenye maana katika malengo ya pamoja. Elimu iliangaliwa kama mchakato ulio kamilika unaohusisha ukombozi na maendeleo ya ufahamu na moyo, mwili na roho, na hivyo kuwawezesha watu wote kutimiza wito wao kikamilifu kama raia wema.

Walutheri wanaamini kuwa utawala wa haki na uwajibikaji ndani ya kanisa na jamii ni ufunguo wa mjadala mkubwa. Wakati wa karne zilizopita mjadala huu kwa Walutheri ulilenga hasa mamlaka za serikali, lakini leo katika dunia ya kidemokrasia na watu wengi wenye mitazamo tofauti mjadala umehama na kukubali wajibu wa msingi wa asasi za kiraia na wa watu wanaoshiriki kwenye matukio ya umma.

Walutheri wanashiriki katika mambo yaliyo kwenye sehemu za umma, si kwa uwezo wa mtu mmoja mmoja tu, bali pia kama jumuiya nzima ya watu waaminio. Kila wakati makanisa ya Kilutheri yameshiriki katika mambo ya jamii kubwa kwa njia ya maneno na matendo. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1947, Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) limekuwa likitoa matamko na maazimio kuhusu mada mbalimbali kwa njia ya vyombo vyake vya kiuongozi. Azimilo la kwanza la Mkutano Mkuu wa FMKD uliofanyika Lund, Sweden, ulijikita katika utetezi wa "watu wasio na makazi na waliohamishwa toka kwenye makazi yao na wakimbizi bila kujali asili, lugha, taifa, au hali."[1] Ilizitaka serikali zote za kitaifa na Umoja wa Mataifa kuunga mkono uhuru wa dini au imani. Kuanzia hapo FMKD limeendelea kuchapisha matamko kuhusu mada fulani au changamoto fulani, likiweka pia mapendekezo ya namna ya kukabili changamoto hizo kwa makanisa shirika na wale wenye maamuzi ya kisiasa katika ngazi tofauti. Uwepo wa kanisa kwa vitendo sehemu za umma unajumuisha mawalisiliano ya kidini kama vile kuhubiri, na mawasiliano ya kidunia kama vile matamko kwa umma na namna tofauti za kufanya utetezi. Hatua zinazochukuliwa na kanisa ni kuanzia kuingilia kati na kutetea wanyonge kwa njia ya diakonia na kwa njia ya ushiriki wao kwenye jumuiya ili kutatua matatizo yao na kuleta amani na haki na kuleta mabadiliko ya kitaasisi katika ngazi za nchi na kimataifa.

Kila kanisa lina mwelekeo wake kihistoria kwa namna lilivyojihusisha sehemu za umma. Kuna sababu nyingi toka nje zinazoathiri namna makanisa yanavyojihusisha sehemu za umma: kanuni za kisheria zinatoa nafasi namna jumuiya za dini zinavyoweza kujipanga zenyewe na kuhusiana na jumuiya zingine ambazo zinajihusisha na mabadiliko chanya sehemu za umma. Zaidi ya hayo, hali ya uwingi au uchache wa watu unashawishi ukubwa wa hatua zinazochukuliwa na jumuia za dini. Sababu nyingine kuhusiana na uwakala wa kanisa kwa umma ni ukaribu au umbali na wahusika katika anga zingine za kijamii, kama vile tamaduni, uchumi, siasa, vyombo vya habari, na jamii ya wasomi. Ni wazi kwamba uwakala wa kanisa katika jamii hautegemei tu namba ya watu, kwa kuwa kuna mifano mingi ya waumini wa dini walio wachache kwa ubunifu wao wameweza kuleta matokeo chanya katika jamii zao.

Katika mazingira fulani, makanisa yameongozwa na wito kutoka kwa nabii Yeremia. "Tafuteni ustawi wa mji huko nilikowatuma uhamishoni, na mkauombee kwa Bwana kwa niaba yake, kwa kuwa katika ustawi

[1] The Lutheran World Federation, *Proceedings of the Lutheran World Federation Assembly* [Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, Mijadala wakati wa Mkutano Mkuu], *Lund, Sweden, Juni 30 – Julai 6, 1947* (Philadelphia, PA: The United Lutheran Publication House, 1948), 92.

wake mtaupata ustawi wenu" Yer 29:7. Wito huu umeyafanya makanisa kutafuta mahusiano kwa nguvu zote na jumuiya zingine kwa ajili ya ustawi wa watu wote. Mahali ambapo makanisa yamejiimarisha, onyo la Paulo la kutoendana na jinsi dunia inavyotaka limekuwa ukumbusho muhimu kwa ajili ya ushuhuda wa makanisa: "Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Rum. 12:2).

## Lengo na muundo wa andiko hili

Katika kusherehekea yubile ya miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa, andiko hili linatafuta kwa nguvu kuelezea ushiriki wa kanisa katika jamii kama itikio lake endelevu la uhuru tulio nao katika kumpenda na kumhudumia jirani. Katika ushiriki huo mawazo yaliyotokana na Matengenezo ya Kanisa yalizaa matunda kuhusu mtizamo wa injili, kanisa na jamii. Tunapoangalia kwa pamoja kuhusu baadaye ya ushirika wa kimataifa, waraka huu unatoa wito kwa FMKD na makanisa wanachama kuzidisha ushirika katika mambo ya umma.

Katika sehemu ya kwanza, andiko hili linaeleza kwa kifupi maana ya tabia ya wazo la sehemu za umma, na kuendeleza wazo kuwa sehemu za umma zingeeleweka kuwa "ni mahali pa haki kwa wote." Inaangazia jinsi uwepo wa kanisa na shughuli zake unaweza kuchangia uwepo wa sehemu za umma ambazo ni jumuishi, zenye kutenda haki na kuleta amani.

Sehemu ya pili inaelezea hoja ya kitheologia kwa ajili ya ushiriki wa kanisa kwa umma kwa mtizamo wa Kilutheri. Wito wa kiubatizo unaangaliwa kama msingi wa kanisa wa ushiriki wake katika jamii. Kwa njia ya imani tunashiriki kuwa Mungu anatukomboa sisi kwa neema. Imani hii inatoa upeo mwingine unaotaka tuone ustawi wa wote kama kusudi la Mungu kwa ajili ya dunia hii na inatupa uhuru wa kumhudumia jirani aliyemhitaji bila ubinafsi. Andiko hili linapitia mawazo na changamoto zinazohusiana na wazo la kitheologia la falme mbili, ambazo pia zinaitwa mamlaka mbili.

Katika sehemu ya tatu, tabia ya ushiriki kwa umma unaainishwa ukihusianishwa na utatu ulio katika 1 Wakorinto 13: imani - tumaini - upendo. Makanisa yanaitwa kushiriki uchambuzi, utambuzi, na uchukuaji hatua ili kutambua eneo linalotakiwa kutoa kauli na kutenda, na kutambua ni nani wa kushirikiana naye na nani ni wa kumpinga.

Sehemu ya nne inaonesha kwa njia ya mfano namna FMKD lilivyouishi ushiriki wake kuhusiana na mambo matano ya umma yaliyoorodheshwa hapo juu. Zaidi hayo, unaorodhesha jinsi vipimo vitatu vya msingi; matendo, mawazo na mifumo, vihusianishwe wakati makanisa yakichangia uboreshaji wa sehemu za umma kama sehemu ya haki kwa wote.

Sehemu ya mwisho inajumuisha mawazo muhimu ya andiko hili kwa kupendekeza “ABCDE” kuboresha uhusika wa kanisa kwa umma.

Kila kipengele kinaweza kutumika kama nyenzo kwa ajili ya kuchambua mwelekeo wa kanisa au umma wote katika muktadha wa msomaji. Maswali matatu baada kila kipengele yamewekwa kuongoza tafakari.

# Sehemu za Umma kama Mahali pa Haki kwa Wote

## Mahali pa haki kwa wote

Lengo letu kama Wakristo ni kufanya maeneo yote ndani ya sehemu za umma yafikike na kila mtu kwa uhuru, bila kuweka tofauti ya aina yo yote, kama vile tofauti ya rangi, tabaka, dini, au jinsia. Hii ina vionjo vyote vya kimwili na kijamii: sehemu za umma ni mahali ambapo watu wote wanazifikia kinyume na sehemu ambazo zinamilikiwa na mtu na kwa hiyo, zinaweza kuwa mahali ambamo jumuiya zote za kijamii zinashirikishana mawazo, rasilimali, ukosoaji na kuhabarishana mambo mbalimbali. Katika hali ya kimaumbile, eneo la mbuga, kwa mfano, kimsingi ni eneo wazi. Linaweza pia kuwa sehemu ya watu kujumuika au watu kuandamana kisiasa na hivyo kuwa na matumizi ya mawasiliano kwa kijamii.

Sehemu za umma zinaweza kuwa sehemu za uwezeshaji wa kijamii pale ambapo makundi ambayo yametengwa na michakato ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi yanafanya sauti zao zisikike na madai yao yatatuliwe na umma na hivyo kuwa na uwezo wa kuchangia katika kutengeneza sera za umma na mabadiliko ya kitamaduni. Katika miongo iliyopita, wanaharakati wapya katika jamii wameleta mabadiliko na kuwezesha matatizo ya kijinsia-kike, kiuchumi, kimazingira, kitabaka na ubaguzi wa rangi kutambuliwa.

Sehemu za wazi ambazo ni jumuishi na shirikishi ni matokeo ya anga mbalimbali za umma zinazokuja pamoja katika anga moja zikiwa na umiliki na hali ya kuwa pamoja. Mawasiliano yaliyopo kijamii, yanawezeshwa na mwingiliano wa sehemu tofauti za umma yakiwakilisha mahitaji na matatizo mbalimbali, na yana mchango mkubwa wa kidemokrasia katika kujenga mawazo ya umma na nguvu ya pamoja katika kupigania haki. Katika kukabili na kutambua mawazo tofauti, madai na matarajio haya, jamii inakuwa imepewa zana nzuri ya kufanya kazi kuelekea ustawi wa watu wote. Mambo matatu ya msingi yanaainisha sehemu za umma kama sehemu ya haki kwa wote:

- Usawa katika kuyafikia mahitaji muhimu na ushiriki katika michakato ya maamuzi ya kisiasa.
- Usalama, na hasa wa watu wanaoishi katika mazingira hatarishi.
- Ushiriki mzuri na uhusiano wa makundi yote katika jamii.

## Sehemu za umma - uhalisia wake

Sehemu za umma jumuishi zinaruhusu upataji wa mahitaji muhimu na ushiriki sawa, na wale wanaoingia sehemu hizo wanatakiwa wajisikie kukaribishwa na kujisikia kuwa salama. Hata hivyo, uzoefu halisi wa watu sehemu za umma, mara nyingi umeonesha kilio cha watu kuwa mbali na ukweli huu.

- Jamii za kienyeji katika nchi nyingi zinapigania kupata haki na kutambuliwa utu wao. Wanapigania haki zao kwa ajili ya kupata ardhi na mahitaji muhimu katika maisha yao na wanalenga kupambana na umaskini kwa kupata huduma sawa zinazotolewa na umma.

- Watu wenye ulemavu wanaendelea kupata matatizo sehemu za umma kwa kuwa wanakosa nyenzo muhimu kuyafikia majengo na kupata nafasi kwenye usafiri wa umma, na kwa sababu hiyo hawawezi kutumia haki yao ya kisiasa na kiuchumi.

- Ubaguzi na matabaka ni ukweli unaodumu na vimepelekea unyanyasaji na unyanyapaa kwa wanyonge na kusababisha kujirudia kwa vitendo vya ukatili, uharibifu na vifo.

- Hakuna usalama wa kutembea kwenye mitaa hasa kwa makundi ya wanawake na wale wanaoonekana kuwa ni tofauti na wengine.

- Hali mpya imeanza kujitokeza katika jamii ya uchokozi dhidi ya watu wa mahusiano ya jinsia moja, na watu walio na jinsi zote.

- Matendo mbalimbali ya kukosa uvumilivu kwa sababu za kidini yanazifikirisha jamii nyingi, na kukosekana kwa sheria au sheria hafifu za kulinda uhuru wa dini au imani unazuia watu kuwa na nafasi sawa.

- Makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na ya wachache hayana uwezo wa kupata mahitaji yao muhimu na yamekuwa hayatendewi haki yanaporipotiwa katika vyombo vya habari.

- Umma unashambuliwa na matangazo yanayoonesha ubora wa mwili usio na uhalisia na itikadi ya ulaji wa vitu usioendelevu.

Nguvu ya kudanganya, kutawala na kunyonya vipo ndani ya mzizi wa ubaguzi. Hali hii inaleta uwepo wa hali isiyo sawa na inawaweka watu katika mazingira hatarishi na ya kikatili. Kuna makundi yasiyotiliwa maanani au kutengwa kwenye mijadala ya umma na mahitaji yao hayatatuliwi ipasavyo na

yanabaguliwa sehemu za umma. Ubaguzi unahusiana sana na kukandamiza makundi fulani kwa njia za kisiasa, kiuchumi kitamaduni, nguvu za kidini, na au nguvu za vyombo vya habari. Ubaguzi unaweza kutokea kwa njia ya unyanyapaa. Katika hali kama hii itaonesha watu wanashirikishwa katika mambo ya umma, lakini ushiriki wao utakandamizwa au kutishwa.

Mawasiliano ya kikatili, udanganyifu na utishaji zinafanya kila mara tuangazie hitaji letu la kupambana ili kupata nafasi ndani ya umma kwa ajili ya watu wote, ambapo watu wenye utambulisho tofauti wanaweza kuwa na mahusiano ya amani na yenye maana kama watu sawa na huru. Kuchukua hatua ndani ya umma kunakuja na wajibu wa kudumisha na kuwezesha tabia ya kukaribisha, kutobagua na kuwa na mahusiano mema.

Kupata njia bora za kutatua migogoro sehemu za umma ni muhimu. Zipo sauti zinazotaka kutia sumu sehemu za umma na kutoa maneno ya chuki kunadhofisha ushiriki wa pamoja wa umma. Uzoefu huu unaamsha wito kwa ajili ya kuweka mfumo ambao utawezesha mazungumzo huru, yenye maana na yenye kuleta amani sehemu za umma. Hili linapaswa kuendelezwa na kusaidiwa na maadili na mahusiano ndani ya umma.

## Mipaka inayobadilika

Tofauti anga ya umma na kibinafsi haiwezi kutumika katika uhalisia wake. Anga ya umma ya jamii ni mwendelezo wa mtu na jumuiya. Kutoka katika nyumba zetu na makanisa tunaenda kuhusiana na umma kwa njia ya mitandao ya kijamii, mazungumzo katika makundi madogo madogo na katika matukio mbalimbali ya kidini. Tunashiriki katika mambo yanayosababisha maisha yetu si tu kama kundi, bali pia kama mtu binafsi. Mipango ya kijamii inayotoa majibu ya mahitaji muhimu ya chakula, malazi, na nguo, haki ya kufanya kazi, afya na elimu yaathiri moja kwa moja maisha yetu ya kila siku. Mipango hiyo inaamua masaa ya kutumia kwa ajili ya familia zetu, namna tuvyojisikia salama wakati wa ugonjwa na ajali na namna tuvyoweza kutoa matarajio kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mipaka ya umma inabadilika na inategemea mazungumzo ya kila mara. Tunapotoa maana ya sehemu za umma kama anga ambazo zinafikiwa na wote kinyume na sehemu zinazomilikiwa na watu binafsi, ni lazima tujue kwamba haki ya kumiliki si ya asili, lakini inaweza kudumishwa na msaada wa watu. Vivyo hivyo, tunakumbushwa kuwa anga kama nafasi ya mawasiliano ambamo jamii inapeana mawazo na kupashana habari na mambo kujadiliwa sana na umma, si tu yanahusu maisha ya wote bali pia ya mtu mmoja mmoja, vikundi vidogo vidogo na vyama.

Utunzaji wa mazingira na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi, kwa mfano, ni masuala ya umma yanayotuhusu sisi wote, na yanahitaji

tuchukue hatua katika ngazi ya mtu mmoja, asasi za kiraia, na serikali za nchi. Katika sehemu za umma, tunakuza uelewa na kupata habari mpya kuhusu changamoto za uchafuzi wa mazingira, upatikanaji wa maji safi na salama, unyonyaji wa watu na rasilimali za umma na na hivyo kuwa na mapatano ya pamoja ya utekelezaji wa mtu au taasisi au serikali za nchi zote katika kukabiliana na changamoto hizi.

Mifumo ya kifamilia, maisha binafsi na ukaribu vinatafsiri nyajibu za kijinsia kwa wanawake na wanaume. Nyajibu hizi zina umuhimu kwa maisha ya mtu na umma, na haviwezi kuwekwa kwenye anga moja. Mtizamo wenye kuweka mpaka madhubuti kati ya sehemu binafsi na umma umetumika kumfanya mwanamke kuwa ni wa kukaa nyumbani na umemzuia kuingia katika nafasi za elimu, siasa na uongozi katika ngazi za juu za kidini. Tafsiri hafifu ya umma na binafsi, inayoainisha tabia ya mahusiano ya viwili hivyo, imesadia kuwa na mtazamo makini wa kutambua mahusiano ya kisiasa yanayofichika na kandamizi ndani ya utambulisho wa kijinsia na kihistoria ya kuwabagua wanawake wasije kwenye michakato ya umma ilikujikomboa, na badala yake wabaki katika maeneo binafsi (kama watumishi wa nyumbani tu).

## Makanisa kama sehemu ya umma

Makanisa ni kipimo cha umma, kwa kuwa yameitwa na kutumwa kuwa wakala wa mabadiliko katika dunia. Kwa kupitia dhamira yao ya lengo la pamoja makanisa yanachangia katika maisha ya umma. Hii haitokani tu kwa kusema na kutenda nje ya mipaka yake, bali pia kwa jinsi yanavyotenga nafasi ndani ya kanisa. Washarika kanisani mara nyingi wanatoka katika hali tofauti, kama vile, kiumri, jinsia, elimu, daraja la kijamii, rangi, tabaka, mielekeo ya kijinsia, na ukabila. Katika hali ya utofauti hizi za kipekee, makanisa wanachama yanapata nafasi muhimu ndani ya kanisa kujadili changamoto zinazoathiri jamii zao kwa ujumla. Si tu kwa njia ya mimbara, bali hata katika vikundi vidogo vidogo, watu wanaweza kuwa na nafasi ya kuongea kuhusu mambo hayo wanapoona kunakosekana uvumilivu wa kidini au kukosekana kwa usawa kwa misingi ya jinsia, rangi, tabaka na uchumi ndani ya kanisa lao na jamii kwa ujumla.

Licha ya kutoa fursa kuwasilisha mambo yenye shida, makanisa pia yana nafasi ya uwepo wake unaoonekana katika jamii. Sehemu za ibada, zinachangia kuumba geografia ya sehemu za umma. Mila na desturi za kanisa zinaonekana, na milio ya kengele za kanisa inasikika pia kwa wapita njia. Makanisa yanaweza kutoa hifadhi ya malazi kwa wale wanaotafuta amani na utulivu na kwa wale ambao sehemu za umma ni kama nyumbani kwao.

Wakati jumuiya za kanisa zikishiriki kwa vitendo ndani ya sehemu za umma zinakutana na watu na makundi ya imani zingine na mitazamo tofauti. Hawa wanatafuta kutatua matatizo ya pamoja kwa lengo la kuchangia katika ustawi wa pamoja. Haki na amani ni vipawa vya Mungu, si tu kwa wale wanaokutana ndani ya kanisa, bali kwa uumbaji mzima. Wakristo wanaitwa kushiriki katika misheni ya Mungu inayoleta uzima tele kwa wote - na si kwa washiriki wa kanisa tu. Makanisa yakijitenga kutoka kwenye matatizo mtambuka ya jamii zao wanapoteza nafasi ya kuwa chumvi na mwanga wa dunia (Mt 5.13—16). Ndani ya Kristo Mungu anakumbatia udhaifu na mateso yetu na analeta upya wa maisha. Ndani ya Kristo Mungu anakumbatia udhaifu na mateso yetu na analeta upya wa maisha ya mwanadamu. Makanisa yanahamasishwa na Mungu kutoka nje ya kuta za kitaasisi na kukaa kinabii katikati ya vilio na matumaini yanayoakisi mahitaji ya mazingira yao na ya kimataifa.

**Maswali kuhusu nguvu ya umma**

- Ni sehemu zipi muhimu na zenye nguvu kwenye umma na ni mambo gani ya umma yapo katika mazingira yako?
- Nani ni wahusika maarufu na ambao sauti zao zinahitajika kusikika zaidi?
- Tutawezaje kuboresha mazungumzo ya umma?

# Kuwa Kanisa katikati ya Umma—Mtazamo wa Kilutheri

## Tumeokolewa kwa Neema - Wito unaotokana na ubatizo wetu

Kama kanisa tunajihusisha katika mambo ya umma —si tu kwa sababu ya imani yetu, bali kwa kuhamasishwa na imani yenyewe. Karama za ubatizo na Ushirika Mtakatifu vinaongoza na kuimarisha ushuhuda wa kanisa ndani ya sehemu za umma. Kipawa cha ubatizo kinaunda kanisa kama jumuiya; kinatoa agano la kipekee kati ya Wakristo na kati ya makanisa.

Ubatizo unamkiri Mungu wa neema asiye na masharti, muumba wa vyote, anayeufanya upya uumbaji katikati ya dunia hii, na anayewategemea wanadamu kutengeneza njia ya Mungu. Mungu wa Utatu anaonesha upendo usio na kikomo katika njia za kushangaza. Mungu kufanyika mwili katika Yesu Kristo hutukumbusha habari ya namna Kristo alivyoingia katika dunia hii na kujishusha (Wafilipi 2). Njia ya msalaba inageuza njia zetu wanadamu kuwa chini-juu, unahoji majivuno, nguvu na kujiinua, na unafungua njia mpya ya uwepo wake ndani ya dunia hii.

Ubatizo unalifundisha kanisa kuwaheshimu watu wote kama watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu na kujaliwa utu ulio sawa. Tukiwa na hakika kuwa Mungu ametupatanisha na yeye, tunakuwa tumekombolewa na tunatakiwa kuwajali wengine. Katika makala yake ya *Uhuru wa Mkristo* Luther anaeleza bayana hili kama ifuatavyo:

> Mkristo ni bwana juu ya vitu vyote, na hayuko chini ya mtu.
> Mkristo ni mtumwa wa vitu vyote na yuko chini ya kila mtu.[2]

Kwa kutamka kwa furaha kuwa kila mtu "anayetoka ndani ya maji ya ubatizo"[3] ana ushirika wa moja kwa moja na Mungu, utamaduni wa Kilutheri unaweka

---

[2] Martin Luther, *The Freedom of a Christian,* [*Uhuru wa Mkristo*] tafsiri yake na Mark D. Tranvik (Minneapolis: Fortress Press, 2008), 50.

[3] Martin Luther, "To the Christian Nobility of the German Nation. Concerning the Reform of the Christian Estate, 1520 [Kwa Watawala Wakristo ndani ya Taifa ya Kijerumani. Kuhusu Matengenezo ya Milki ya Kikristo, 1520]", ndani ya kitabu cha Helmut T. Lehmann (ed.), *Luther's Works* [*Kazi za Luther*], vol. 44 (Philadelphia: Fortress Press, 1966), 129.

mkazo kuwa kila aliyebatizwa ameitwa na kuwezeshwa kushiriki katika hali zote za maisha ya kanisa (1 Pet 2). Mungu ambaye ni Roho Mtakatifu anamwaga karama kwa kanisa zima (Efe 4:11-13; 1 Kor 12:4-11), na anawaamsha wanaume na wanawake kuchangia katika kuitunza jumuiya. Hivyo kanisa zima, na kila msharika, wanashiriki katika ushuhuda wa kanisa kwa umma. Mioyo yote, akili na mikono vinahitajika kwa ajili ya jukumu la kanisa la kushirikishana maono ya Mungu kwa ajili ya dunia hii na kupaza sauti dhidi ya uonevu. Ubatizo una maana ya wito kwa ajili ya maisha yenye imani, matumaini na upendo, na utayari wa kumhudumia jirani na kujali ustawi wa watu wote. Kwa hiyo, ubatizo ni msingi wa ushiriki wa Kikristo kwa mambo yote ndani ya kanisa na sehemu za umma.

Karama ya Ushirika Mtakatifu inadumisha na kuimarisha jumuiya ya kanisa. Ni ukumbusho wa kila wakati wa upatanisho ambao Kristo aliuleta kwa dunia nzima, na anawaita Wakristo kuwa mabalozi wa dunia iliyopatanishwa (linganisha 2 Kor. 5:20).

Karama za ubatizo na Ushirika Mtakatifu vinaunda na kuimarisha kanisa kama jumuiya ya Neno la Mungu. Kwa pamoja zinaonesha kuelekea msingi wa wito wa kanisa, yaani misheni yake kamili katika kutanganza, kuhudumia na kufanya kazi za utetezi, ili kanisa liwe sauti ya umma pale lilipo. Mazingira tofauti ya kuongea na kutenda ndani ya umma - ndani ya kanisa na ndani ya jamii au vyote kwa pamoja - vinahitaji kutofautishwa na kuhusianishwa kwa umakini. Kwa msingi huu, wazo la milki mbili zilizoasisiwa na utamaduni wa Kilutheri linatoa mwongozo wa baadhi ya mitazamo.

## Tofauti kati ya milki ya kiroho na kidunia

Katika theologia ya Kilutheri kutofautisha kati ya milki za kidunia na kiroho kumetoa mchango mkubwa. Luther alikosoa kwa nguvu uingiliaji usiotakiwa wa mamlaka za kidunia katika mambo ya kiroho, na mipango isiyohitajika ya watendaji wa kidini katika mambo ya kidunia. Katika tafakari yake kwa mamlaka za kidunia, Luther anaelezea kwa ufasaha maana za upeo wa milki zote mbili na kuoneshamipaka ya kila mmoja.[4]

Istilahi ya mafundisho ya "milki mbili" imebadilishwa na kuwa istilahi ya "tawala mbili" au "dola mbili." Dola ya mwisho inaonesha njia mbili, jinsi Mungu anavyoitawala dunia au njia mbili ambazo Mungu anaitunza dunia: na katika moyo wa dola ya kiroho ni uwepo wa kutendewa haki kwa njia

[4] Martin Luther, "Temporal Authority: To What Extent it Should be Obeyed [Mamlaka ya Kidunia: Ni kwa Kiwango Gani Watu Waitii]" [1523], katika andiko la Helmut T. Lehmann (ed.), *Luther's Works [Kazi za Luther]*, vol. 45 (Philadelphia: Muhlenberg Press, 1962), 77-129.

ya kushirikishana habari njema ya Mungu kwa uumbaji wote. Katikati ya dola ya kidunia tunaona mahangaiko kwa ajili ya haki na ujenzi wa misingi ya sheria inayowahakikishia watu amani katika jamii.

Luther anaiita dola ya kwanza ya Mungu kuwa "kazi halisi" (*opus proprium*) kwa sababu kueneza injili kunaelezea asili halisi ya Mungu, ambayo ni upendo. Dola ya pili, hata hivyo, ni "kazi ya nje" (*opus alienum*) kwa sababu inahitajika kwa ajili ya sababu zilizo nje, hasa sababu ya dhambi ya mwanadamu inayosababisha machafuko yenye uharibifu katika jamii.

Katika utawala wa kidunia, sheria zinatumika kuweka mifumo na maagizo katika jamii ili watu wote waweze kuishi kwa pamoja na kwa amani. Sheria zinatekelezwa na mahakama; hizi ni za lazima kwa sababu ya ukweli wa dhambi na makosa. Bado, dola hii inahamasishwa na upendo wa Mungu kwa sababu ni sehemu ya mpango wa Mungu wa kuitunza dunia *(conservatio mundi)*: Mungu hawaachi wanadamu peke yao na maovu waliyoyatengeneza. Lakini sio maelezo ya moja kwa moja ya upendo wa Mungu, kwa kuwa mamlaka zinahitaji ziwe na ustadi na uwezo wa kuamuru watu kutii sheria au kutumia nguvu kukabili fujo.

Milki ya kiroho inarejea utawala wa Mungu kama uumbaji mpya uliopatanishwa, ambao unaanza kujidhihirisha wenyewe ndani ya jumuiya ya waaminio. Hakuna mahakama zinazohitajika hapa kwa sababu hii itapingana na tabia ya utawala wa kiroho. Kwa hiyo, tofauti kati ya milki mbili ina maana ya ukosoaji wa kila jaribu la kushabikia kueneza injili kwa njia ya kutumia nguvu za nje. Kipengele cha 28 cha Ungamo la Augsburg kinasisitiza kuwa maaskofu wanatakiwa kuhubiri injili "si kwa nguvu za kibinadamu, bali kwa njia ya Neno la Mungu tu"[5] *(sine vi humana, sed verbo).* Hii inaelezea hali ya tabia ya kazi ya kanisa: ambayo ni kushawishi, na si kulazimisha.

Lazima tukubali kuwa pamoja na mawazo haya mazuri ya kitheologia ya kutofautisha kati ya milki mbili, mawazo ya uhuru wa kidini na uvumilivu hayakutiliwa mkazo katika karne hii ya kumi na sita. Walutheri walioongoza matengenezo pia walichangia kutenda vitendo vya kukosa uvumilivu na kuwatesa wana matengenezo wenye siasa kali, hasa waliopinga ubatizo wa watoto wadogo na waliwashambulia pia kwa mdomo na maandishi Wayahudi, na mashambulizi hayo yameendelea kuwa nguvu kwa karne zote - ingawa yamepingwa katika miongo ya karibuni kwa njia ya kutafuta toba na upatanisho.[6] Kwa sababu ya michakato hii tumekuwa makini

[5] "The Augsburg Confession [1530], [Ungamo la Augsburg]" na Robert Kolb and Timothy J. Wengert (eds.), *The Book of Concord. The Confessions of the Evangelical Lutheran Church* [Kitabu cha Concordia. Maungamo ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri] (Minneapolis: Fortress Press, 2000), 94.

[6] Mwaka 1984, FMKD katika Mkutano Mkuu wa Budapest ulileteWa kauli za Luther, "Luther, Ulutheri na Wayahudi." Walutheri walipokea maneno ya Luther ya kuwakataa Wayahudi na

zaidi na hatari ya kujipinga wenyewe katika mafundisho na matendo yetu. Tunathibitisha kuwa suala la kupinga uovu liendelea kuwa jukumu muhimu na endelevu kwa kauli mbiu hii "si kwa nguvu za kibinadamu, bali kwa njia ya Neno la Mungu tu" *sine vi humana sed verbo* ichipushe nguvu yake kamili ya kupinga uovu katika jamii.

## Changamoto ya namna ya kuendana na tofauti hizi

Mungu anatawala milki zote, ya kidunia na ya kiroho. Hii ina maana kuwa hakuna jambo halisi lililo nje ya ufahamu wa ahadi ya Mungu kwa dunia hii, na hakuna jambo halisi nje ya upeo wa Mungu. Kanisa linaitwa kuwasilisha upendo wa Mungu kwa dunia kwa neno na matendo. Kwa hiyo, kanisa linaposhuhudia uonevu na ukandamizaji katika enzi ya kidunia, linahitaji kupaza sauti, kuwawezesha wanyonge, kuwahudumia wenye uhitaji na kuwalinda walio katika mazingira hatarishi.

Tofauti kati ya dola mbili za utawala wa Mungu ina nguvu ya hoja na udhaifu wake. Kwa mfano, wazo hili limetumika vibaya kupendekeza kwamba kanisa la kweli la kiroho si lazima lijihusishe na mambo ya umma ili libaki safi na timilifu. Zaidi ya hayo, limehimiza utii wenye upofu katika mazingira ambamo kanisa lingetakiwa lipinge uovu kutokana na imani na lengo lake.

Kwa upande mwingine, moja ya nguvu ya kutofautisha milki mbili ni kwamba inasaidia kuelewa namna tunavyoweza kuhusiana na watu nje ya kanisa katika uwanja wa umma bila kuwataka watu wawe Wakristo. Wakati huo huo, dhana ya dola mbili haituhamasishi sisi kuacha imani

---

maneno yake makali dhidi ya Wayahuhidi kuwa wenye dhambi, na waliapa kuondoa hali yoyote ya dhambi inayolingana na hiyo ndani ya makanisa yao au baadaye. Angalia maandiko kwenye kiambatisho ya: Wolfgang Greive and Peter Prove (eds.), *A Shift in Jewish-Lutheran Relations? A Lutheran Contribution to Christian-Jewish Dialogue with a Focus on Anti-Semitism and Anti-Judaism Today* [*Ni Mabadiliko katika Uhusiano wa Uyahudi-Ulutheri? Mchango wa Ulutheri katika Mazungumko kati ya Wakristo na Wayahudi yakilenga Kuondoa Upinzani dhidi ya Wasemitiki na Wayahudi katika Dunia ya Leo*], LWF Documentation 48 [Waraka wa FMKD 48] (Geneva: LWF, 2003), 196, angalia **www.lutheranworld.org/sites/default/files/dts-doc48-jewish-full.pdf**.

Kuhusiana na mateso ya Waanabaptisti, na uungwaji mkono wa mateso haya na wanamatengenezo, FMKD katika Mkutano Mkuu wake wa Stuttgart 2010 liliomba msamaha, "kwa Mungu na kwa ndugu zetu wa Mennonite." Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani, *Utupe Leo Mkate Wetu. Taarifa Rasmi. FMKD Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja Stuttgart, Germany, 20-27 Julai 2010* (Geneva: The Lutheran World Federation, 2010), 47f. **http://assembly2010.lutheranworld.org/uploads/media/Mennonite_Statement-EN_04.pdf** Wawakilishi wa Mennonite waliwapokea Walutheri kwa mikono iliyonyooka na kusema "Kwa furaha na kwa unyenyekevu tunaungana na Mungu kuwasamehe" The Mennonite representatives received the Lutherans with open arms and said "We joyfully and humbly join with God in giving forgiveness" (andiko hilo hilo, uk 50). Pande zote ziliahidiana kuwa na mahusiano ya karibu na ya ndani.

yetu kwa sababu ya umma. Kwa njia hii, tofauti inatoa fursa elekezi kwa ajili ya kuuishi wito wa Kikristo katika jamii yenye dini mbalimbali.

Nguvu nyingine ya dhana hii inakaa katika nguvu yake ya kuchunguza mahusiano magumu kati ya dini na siasa. Luther aliwashauri watawala kuhusu mambo kadhaa ya kisiasa. Hakufanya kosa la kuhukumu vibaya hali ya kisiasa, ili isimzuie kutoa ushauri. Leo, kama ilivyokuwa wakati wa Luther, jukumu hili limejawa na sintofahamu nyingi. Kanisa linahitaji kufuatilia mijadala ya umma kwa karibu na kuwa tayari wakati wote kushiriki mijadala hiyo. Bado, wakati huo huo, kanisa kamwe lisipoteze uwezo wake wa kutofautisha kwa usahihi kati ya dola ya kidunia na kiroho. Kutokana na mtizamo wa Kilutheri, juu ya utawala wa ki-mungu, ni wazi kwamba ni lazima upigwe marufuku. Wajibu wa kanisa si kutawala umma wote, bali ni kuuonya dhidi ya mtizamo au dini au Ukristo au dini zingine visiwe katika hatari ya kuwa itikadi ambayo itatawala sehemu ya umma.

Tofauti ya milki mbili ni muhimu kwa ajili ya kutambua wajibu sahihi wa dini kuhusiana na mambo ya kisiasa. Tofauti kati ya sheria na injili vinatumika kama alama katika kutangaza injili ndani ya kanisa. Jukumu la kwanza na muhimu la kanisa ni kutangaza injili; ingawa, ili kufanya hili kanisa linahitaji kuweka sheria na kanuni nzuri. Utamaduni wa Kilutheri unatofautisha kati ya matumizi ya sheria kitheologia na kiraia. Katika matumizi yake ya kitheologia, sheria inamfunua na kumshitaki mwanadamu kama mtenda dhambi. Katika matumizi yake ya kiraia, sheria inalenga kudumisha utaratibu mzuri wa kiraia katikati ya dunia yenye dhambi. Mambo haya mawili ya kutangaza (injili) yanaweka misingi ya umuhimu wa kuweka tofauti sahihi, ingawa mtu bado unaweza kuzihusianisha sehemu hizo, ili kumhusisha Mungu na dunia nzima.

Luther alitambua hatari ya serikali kandamizi. Alitoa wito wa kuchambua kwa kina nguvu za kisiasa, kote ndani ya utawala wa kanisa na utawala wa kidunia. Kwa Luther, utawala wa haki ni kigezo cha kuishi pamoja katika haki na amani. Kanisa ni lazima liziwajibishe mamlaka za kidunia kwa njia ya uelewa wake wa neema ya Mungu na haki. Kwa upande mwingine, kanisa la Kilutheri linapofanya majukumu yake yanayoweza kufanywa na serikali, linatakiwa litafakari kwa makini ni kwa njia gani majukumu haya yanakubaliana na lengo lake la msingi.

Umoja ndani ya utawala mmoja wa Mungu unataka uongozi wenye uwajibikaji na uwazi ndani ya kanisa na hata katika utawala wa kidunia; jinsi makanisa yanavyoshughulikia tofauti na kupanga michakato ya kimaamuzi ni sehemu ya ushuhuda wake kwa umma. Uhalali mkubwa wa kanisa unategemea mambo haya yanayoelekea kutokuwa na mvuto - na ni sawa iwe hivyo. Mifumo ya Kisinodi (kidayosisi) ni mahali pamoja, ambapo wote wachungaji na wasio wachungaji leo wanashiriki ile sehemu muhimu ya uongozi wa kanisa.

Kanisa linahitaji kutambua na kuheshimu kuwa utawala wa Mungu upo kwa vitendo katika dola ya kidunia, na linahitaji kuwa wazi kushuhudia uwepo wa Mungu katika milki ya kidunia. Haki inaunda mfumo muhimu kwa ajili ya kuwezesha ushiriki katika sehemu ya umma. Haki inatoa muundo wa kupambana na tofauti na utofauti kati ya raia na kuhakikisha wako sawa mbele ya sheria. Haki ni nyenzo muhimu kwa ajili ya kuitisha hoja kwenye dhana ya makundi ya wengi dhidi ya makundi ya wachache. Inaruhusu kanisa kuorodhesha na kutambua uonevu, kwa kuzingatia wito wake kama wakili kwa ajili ya watu wote kwa sababu tumeumbwa kwa mfano wa Mungu. Kwa mantiki hiyo kanisa linahimiza kupaza sauti kwa ajili ya wanaokandamizwa, wanaoishi katika mazingira hatarishi na maskini. Kwa hiyo, kanisa linajihusisha na umma kwa njia ya misingi ya mifumo ya kisheria inayoheshimika na linadumisha ubora wa haki za binadamu za kimataifa.

Nini, tena, kwa msingi wa tofauti kati ya dola mbili, je huu ni wito maalumu wa kanisa kuwa sehemu ya kisiasa na umma? Kwanza, makanisa yanatakiwa yapinge dini kuingiliwa na siasa na siasa za kimaeneo. Hali ya kutumia dini na siasa vinafubaza na kusaliti maana na matumizi ya dhana ya dola zote mbili, na yanaleta uharibifu kwa jamii nzima. Pili, makanisa ni lazima yatunze kwa uangalifu mkubwa tofauti kati ya taasisi za nchi na za dini - kwa kuangalia vyote, yaani matumizi yake ya nguvu na matumizi sahihi ya nguvu ya mamlaka zinazotawala. Tatu, makanisa yanatakiwa yaangalie kwa karibu nafasi yao kisiasa, yakijihusisha yenyewe pale yanapohitajika na yakijenga msingi wake katika uelewa wa haki ya Mungu na neema kama vitu vilivyo wazi katika jamii. Nne, makanisa yana nafasi yake katika umma kama mahali yanaposhiriki kuishi pamoja na watu wa imani na misimamo mingine. Katika nafasi hiyo ya pamoja haki za binadamu zinatakiwa kuwa njia ya kuongea lugha ya pamoja. Tunazishukuru haki za binadamu, kwa njia hiyo tunaweza kupata uwanja wa pamoja na kutatua changamoto za kimataifa.

## Maswali kuhusu tofauti ya dola mbili

- Je nini baadhi ya uzoefu wa kanisa lako kihistoria au kwa wakati huu ambapo tofauti katika ya dola ya kidunia na kiroho imefanya kazi au imeshindwa kufanya kazi vizuri? Ni ushawishi upi wa kitheologia au kibiblia unaliongoza kanisa lako kujihusisha na umma wake? Kanisa lako limeweka mifumo ya kiutawala ambayo ni wajibishi na wazi?

- Tunawezaje kuwa na ushiriki wa maana katika mijadala ya pamoja na umma kama vile haki za binadamu na malengo ya maendeleo endelevu?

# Tabia za Ushiriki wa Kilutheri kwa Umma

## Ujasiri na uwazi: Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma katikaimani

Msingi wa dhamira ya Kilutheri ya kuokolewa kwa neema unahusishwa sawia na uelewa wa ndani wa hali ya muumini kuwa ni mwenye haki na wakati huo huo ni mwenye dhambi. Sisi hatuwezi mbele za Mungu, pia tunaendelea kutafsiri vibaya mapenzi ya Mungu. Wakati huo huo, tumejazwa na neema ya Mungu, na bila kujua tunaendelea kutimiza mapenzi ya Mungu. Kukiri mambo haya mawili ni jukumu la waumini wote wa Kilutheri na ukiri huu unaumba uhalisi wa kanisa na pia unamuumba upya muumini mmoja mmoja. Kanisa, na jumuiya ya waaminio, wanatakiwa kukiri uhalisi wa kuwa wenye haki na wakati huo huo kuwa ni wenye dhambi.

Kwa sababu hii, kanisa haliwezi kujiona kuwa lipo katika ngazi ya juu katika mijadala ya umma katika hali ya kudhani kuwa ni mamlaka takatifu. Haki ya Kikristo inatokana na kumkri Mungu kama Mungu, na neema kama zawadi. Wakristo wamekombolewa kwa njia ya neema ya Mungu ili kukiri udhalimu wao na uonevu wa kijamii kama tatizo linalowahusu kama ilivyo kwa jamii yote kwa ujumla wake. Haya ni maelezo kwa umma yenye ujasiri wa uhuru wa kanisa ili kutangaza injili na kuuhudumia uumbaji.

Biblia imetupa changamoto ya kuwa tayari wakati wote kutoa majibu kwa yeyote yule anayetutaka tuwajibike kwa matumaini kwamba yuko pamoja nasi; na tufanye hivyo kwa upole na heshima (linganisha 1 Pet. 3:15 na kuendelea). Kwa hiyo hakuna utata kati ya misheni na kujihusisha na masuala ya umma kama ilivyoainishwa katika andiko hili. Kutangaza injili kimsingi ni juhudi ya umma, iwe ndani au nje ya kuta za kanisa. Kutokana na uelewa wa Kilutheri, ibada za Jumapili ni tukio la umma, hata kama linaelezea kuwa ni jumuiya ya kiroho kati ya washiriki wake wakidhihirishwa kwa njia ya sakramenti. Mahubiri na namna nyingine ya matangazo vinaeneza upendo wa Mungu na uwezo wa neema ya Mungu ya kuukomboa ulimwengu.

Kanisa linategemea kusikiliza Neno la Mungu kwa ajili ya kazi yake ya kuitangaza injili. Katika hali ya habari nyingi za kidini zinazotolewa na njia mbalimbali za vyombo vya habari inaweza kuwa vigumu kutambua sauti ya Mungu. Kwa hiyo, ili kanisa liweze kufafanua Neno la Mungu, tafakari ya kitheologia ni muhimu. Inahusisha kutathimini jinsi kanisa

linavyosoma Biblia na kuelewa mafundisho ya Kilutheri katika dunia ya leo. Kuchambua mazingira ndani ya maeneo yetu ya kimataifa ni sehemu muhimu ya michakato ya kukuza ufahamu wa kitheologia na kimaadili. Uhusika huu kwa njia ya theologia ni chanzo muhimu cha kupata ukweli wakati kanisa linapoushuhudia kwa umma.

## Ustahimilivu na uvumilivu: Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma katika matumaini

"Ni bayana, ufalme wa Mungu unakuja wenyewe bila maombi, lakini tunaomba katika sala hii kuwa unaweza kuja kwetu."[7] Maelezo mafupi ya Luther kuhusu sala ya Bwana katika Katekisimo Ndogo inaweka kipimo cha pili cha ushuhuda wa Kilutheri kwa umma: kipimo cha matumaini katika uvumilivu na shauku ya unabii. Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma umewekwa kwa kufuata mwelekeo mpana wa mwaliko wa Mungu kwenye ahadi ya Mungu ya baadaye. Mtizamo huu wa ufalme wa Mungu unazipa kazi za kanisa uhalali wa kweli na maana nzito, lakini haiufanyi ufalme wa Mungu utegemea kazi za kanisa. Kwa mantiki hiyo hiyo, ushuhuda wa Kilutheri kwa umma unaongea katika roho ya utulivu na uwajibikaji. "Mafanikio" yake hapo mwishoni hayalitegemei kanisa pekee wala hali inayofaa ya kisiasa.

Wazo la matumaini linaonesha uwigo wa kiulimwengu wa haki na neema ya Mungu. Ushuhudu wa Kilutheri kwa umma unaangalia ng'ambo ya muktadha wake wa karibu na unatafuta kuwahusishawatu wa mazingira mengine. Makanisa ya Kilutheri yanajihusisha na sehemu za umma katika hali ya upana wake, yakitafuta kuvuka mipaka ya maeneo, tamaduni, na itikadi zao. Kwa njia hii, ushuhuda wa Kilutheri unalenga kupanua upeo wa muktadha wake, ili kuelekea kwenye mjadala mpana zaidi na kutengeneza sehemu mpya za umma.

## Mshikamano na uwezeshaji: Ushuhuda wa Kilutheri kwa umma katika upendo

Kwa njia ya kuishi ndani ya Kristo na kubadilishwa kwa njia ya upendo wa Mungu, tumekombolewa ili kupenda na kuwahudumia wengine. Na, "jirani yangu ni nani?" (Luka 10:29). Jibu la Yesu linavuka uelewa wa kawaida wa jirani na linataka tuondoe mipaka ya kikabila, rangi, mawazo potofu kuhusu jinsia, na hali za kijamii: mahitaji ya mtu mwingine ndio mambo muhimu.

---

[7] "Katekisimo Ndogo ya Martin Luther [1529]," *Katika Kitabu cha Concordia*, op. cit. (nukuu ya 5), 356.

Wito wa kumpenda jirani ni sehemu ya ndani sana ya maisha ya Kikristo. Ni wito wa kanisa kama jumuiya ya waaminio. Unaliongoza kanisa kwenye utetezi na uwakili kwa umma. Kukombolewa kwa neema ya Mungu ili kumpenda na kumhudumia jirani maana yake ni kukiri kuwa na mshikamano na wanyonge katika jamii. Kimsingi, ushuhuda wa Kikristo sehemu za umma unaongozwa kwa njia ya kutathmini madhara ya maamuzi ya kisiasa kwa walio wanyonge sana kwenye jamii. Ushuhuda wa Kikristo sehemu za umma hauelekezwi na mahesabu ya uwingi wa watu wenye ushawishi, bali na hitaji la haki na neema ya Mungu kwa wote.

Sehemu sahihi ya ushuhuda wa Kilutheri ni sehemu zote katikati na pembezoni mwa jamii. Kama viumbe wa Mungu, wanadamu wote wameumbwa kuwa na utu sawa, hivyo kanisa linaitwa kutathmini kwa upya tofauti za kitamaduni kati ya sehemu ya katikati na pembezoni mwa jamii, kati ya wenye nguvu na wanaokandamizwa, kati ya watu wa hali ya chini na ya juu. Kwa kushudia jinsi Kristo alivyofanyika mtumwa kwa ajili ya wanadamu, makanisa ya Kilutheri yanahitaji kujikagua katika kujihusisha kwake na mifumo ya nguvu za kisiasa na kitamaduni.

Mazungumzo na ushirikiano ni muhimu ili kutengeza mazingira ya ushiriki wa umma. Kujenga jumuiya himilivu katika maeneo yetu ni mahitaji ya msingi katika jamii, hasa pale ambapo watu wa hali tofauti wanaishi pamoja kijamii-kiuchumi, kikabila, kidini au misingi ya kitamaduni. Katika roho ya ujirani mwema, sharika ndani ya kanisa zinachangia sana katika kujenga jumuiya na kuvuka migogoro iliyojikita ndani sana na kurithiwa. Ufunguo kuelekea ushiriki wenye usawa kwa wote ndani ya jamii yenye haki na amani ni kutoa elimu yenye kuleta mabadiliko chanya ili watu waweze kuwajibika na mawakala waliokomaa katika familia, jumuiya na jamii zao.

Uwepo wa huduma ya kinabii unauishi uhusiano wa wenye kujali watu wengine, katika hali zote za ustawi wa kimwili na uwezeshaji wa kiroho. Hivyo inaelezea habari nyingi zinazouweka wazi utu wa mwanadamu na kuwa na mshikamano na wanyonge katikati ya mazingira hatarishi, dhambi na mateso.

### Maswali kuhusu tabia ya uhusika wa Kilutheri kwa Umma

- Ni kitu gani kinasaidia au kukwamisha kanisa katika kujihusisha kwa ujasiri na uwazi sehemu za umma?

- Ni kitu gani kinaliendeleza kanisa wakati likiuishi ushuhuda wake kwa uvumilivu na mapenzi mema ya kinabii?

- Ni matendo gani yanayoonekana kueleza mshikamano na uwezeshaji katika kanisa lako na katika ngazi ya sharika na hata ngazi za uongozi?

# Njia Zinazotumika na Kanisa Kujihusha Sehemu za Umma

## Mifano ya kujihusisha na umma

Katika historia yake yote, FMKD limejihusisha na mambo mengi magumu ya migogoro katika umma. Mifano mitano inasaidia kuonesha kwa kifupi kuwa uthabiti, na uhusika wa muda mrefu sehemu za umma ni sehemu muhimu ya maisha ya pamoja kama jumuiya ya kimataifa. Kwa kushirikiana pamoja na kuhusika katika mambo ta umma tunauishi wito wetu kama Wakristo tuliowekwa huru na Kristo ili kupenda na kuwahudumia wengine.

### Mfano 1: Kujihusisha na wakimbizi

Baada ya madhara ya Vita Kuu ya II ya dunia na mamilioni ya watu kuyakimbia makazi yao, FMKD liliitikia kwa vitendo kutatua mahitaji ya watu walioyakimbia makazi yao huko Ulaya. Kuanzia Mkutano Mkuu wake wa kwanza kabisa 1947 mpaka leo FMKD limeweka kuwa kuwafikia wakimbizi ndio mojawapo ya shughuli zake za msingi. Leo kuna wakimbizi zaidi ya milioni 60 duniani, ikijumuisha watu waliokimbia makazi yao, wakimbizi na wanaotafuta hifadhi, na kati ya hao milioni 2.3 wanafikiwa na shughuli za Idara ya Misaada kwa Dunia ya FMKD. Juhudi za makusudi zimefanyika kuitikia dharura ya kusaidia wakimbizi katika nchi nne za Iraq, Syria, Jamhuri ya Afrika ya Kati, na Sudani Kusini.[8]

### Mfano 2: Ushiriki katika kutatua suala ubaguzi

Ilipotokea hali mbaya sana ya ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini, ambao pia uliathiri ushirika ndani na nje ya makanisa, FMKD lilitamka kuwa

---

[8] Makubaliano kati ya FMKD na Shirika la Wakimbizi Duniani mwaka 2014 soma, **www.lutheranworld.org/news/lwf-and-unhcr-sign-memorandum-understanding-humanitarian-cooperation**
"Kukaribisha Mpitaji: Makubaliano ya Viongozi wa Dini," tamka linalojenga misingi na dhamani ya ukarimu ambao upo ndani ya dini kubwa zilizokubaliwa na Halmashauri Kuu ya FMKD katika kikao chake 2013, makubaliano haya utayaona katika tuvuti yake ya **www.lutheranworld.org/sites/default/files/Welcoming_the_Stranger.pdf**

makanisa yaliyojiingiza kwenye mafundisho ya uzushi kutetea ubaguzi wa rangi yamesababisha kujitenga yenyewe kutoka kwenye ushirika. Ubaguzi wa rangi ulichukuliwa kama jambo la kitheologia, kwa kuwa ulikiuka misingi ya kitheologia kama ilivyokuwa imeelezwa kinagaubaga katika tamko la Mkutano Mkuu wa FMKD mwaka 1977 mjini Dar es Salaam.[9]

Mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi wa hali zote yameendelea kuwa jambo muhimu kwa makanisa ya Kilutheri duniani, wakati huo huo FMKD likitoa matamko makali kwa umma kulaani dhambi ya ubaguzi katika mkutano wake wa 2015.[10] Kwa kuwa na uelewa mpana wa miundo iliyofichika ya ubaguzi, makanisa ya Kilutheri pia yanakemea mifumo mingine ya kibaguzi na kutetea mahusiano yenye kujali haki na utamaduni wenye kushawishi kuishi kwa udugu. Kuishi kwa udugu kunazitaka jumuiya na jamii kwa kuzingatia mahusiano ya kukarimiana, kuheshimiana licha ya tofauti zao na uwezo miongoni mwa watu na jumuiya, ambavyo vinastawisha maisha ya pamoja.

## Mfano 3: Kupigania haki ya kijinsia

Kama nyenzo pekee ya kupambana na uonevu unaodumu katika mahusiano ya kijinsia, Halmashauri Kuu ya FMKD lilipitisha Sera ya FMKD ya Haki ya Kijinsia mwaka 2013.[11] Sera hii inajenga msingi wake katika kazi ya uwezeshaji kwa wanawake kwa miongo mingi na ahadi endelevu ya kuwezesha ushiriki wa maana wa wanawake na vijana katika michakato ya maamuzi katika ushirika. Patano la Mkutano Mkuu wa FMKD mwaka 1984 linatoa nafasi ya kuwepo na usawa wa kijinsia wa angalau asilimia arobaini katika nafasi za uongozi katika vyombo vya kimaamuzi na vikosi kazi vya kamati.[12] Kukubaliwa kubarikiwa wanawake kumekuwa ni sharti la msingi la FMKD na hivyo kuwa sehemu ya ndani ya tafsiri yake ya kanisa ndani ya FMKD.

---

[9] "Afrika ya Kusini: Ungamo la Kiutu," tamko la FMKD katika Mkutano wake Mkuu wa 1977: Angalia: Arne Sovik (ed.), *In Christ – A New Community. Official Proceedings of the Sixth LWF Assembly in Dar es Salaam, Tanzania, ¥ 13-25, 1977* [Ndani ya Yesu - Mijadala Rasmi ya Mkutano Mkuu wa Sita Wa FMKD, Dar es salaam, Tanzania Juni 13-25, 1977] (Geneva: The Lutheran World Federation, 1977), 180.

[10] "Dhambi ya Ubaguzi wa Rangi," Tamko la Halmashauri Kuu ya FMKD kwa umma katika Mkutano wake mwaka 2015, angalia **www.lutheranworld.org/sites/default/files/Public%20 Statement%20-%20The%20Sin%20of%20Racism.pdf**

[11] **www.lutheranworld.org/sites/default/files/DTPW-WICAS_Gender_Justice.pdf**

[12] Carl H. Mau (ed.), Budapest 1984. *"In Christ – Hope for the World [Ndani ya Kristo Matumaini kwa Dunia Yote]." Mijadala Rasmi ya Mkutano Mkuu wa Saba wa FMKD,* Ripoti No. 19/20 (Geneva: The Lutheran World Federation, 1985), 224f.

### Mfano 4: Ushiriki katika kutetea haki ya tabia nchi

Kwa pamoja na washirika wake wa kiekumene na dini zingine, FMKD limeendelea bila kuchoka kuelewesha watu juu ya madhara hasi ya kiekolojia na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi kwa jamii. FMKD linapigania kuwa na sera ambazo zitalinda mazingira, kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabia nchi, kuwezesha kumudu hali ya mabadiliko, na kuzuia kuendelea kwa uharibifu wa mazingira. Hatua hizi za FMKD dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi zina historia yake kuanzia Mkutano wake Mkuu wa Sita 1977 pale Dar es salaam. Tangu wakati huo, Walutheri wameoneshakuguswa kipekee na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi, na hasa maskini na wenyeji walio nje ya mifumo ya nchi, kwa njia ya miradi kama *Haraka kwa Ajili ya Kampeni dhidi ya Mabadiliko ya Tabia Nchi*, na ushiriki wake katika juhudi za utetezi pamoja na dini zingine kuelekea Patano la Paris 2015.[13]

### Mfano 5: Kushiriki mazungumzo kwa ajili ya mahusiano ya amani na dini zingine

Katika dunia yenye migawanyiko na ugomvi, pia kati ya jumuiya za kidini, kuwaleta watu wa imani tofauti ili kuimarisha maelewano kati yao na kuwa na ahadi za pamoja kwa masuala wanayoshirikiana kunafanya ushuhuda wa ushirika kuwa mzito. FMKD limeahidi kuendeleza mazungumzo na ushirikiano na dini zingine. Moja ya njia kuu za FMKD katika mahusiano yake na dini zingine ni kushirikiana na washirika wa dini zingine katika kutatua majanga ya kibinadamu wakati likiendelea na mazungumzo ya kitheologia kati ya viongozi wa dini na wasomi.[14]

---

[13] Kampeni ya "Kufunga kwa ajili ya Mazingira" angalia tovuti yake, **http://fastfortheclimate.org/en/** "Tamko la Haki ya Kimazingira," tamko kwa umma la Halmashauri Kuu ya FMKD katika kikao chake cha 2014, angalia tovuti yake ya **www.lutheranworld.org/sites/default/files/Council2014-PublicStatement_ClimateJustice.pdf** na tamko la 2015, angalia **www.lutheranworld.org/sites/default/files/Public%20Statement%20-%20Advocacy%20and%20Action%20for%20Climate%20Justice_0.pdf**

[14] Tamko la Pamoja la Kuleta Amani, Demokrasia na Maendeleo, Mei 2014, Dar es Salaam angalia tovuti ya **www.lutheranworld.org/sites/default/files/Interreligious_Declaration-DaresSalaam_8May2014.pdf** Mawasilisho ya Kongamano la Mazungumzo na Dini Zingine "Maisha ya Dini na Umma huko Asia," Septemba 2015, Hong Kong, **www.lutheranworld.org/sites/default/files/interfaith_consultation_communique_0.pdf**

Ushirikiano kati ya FMKD na Shirika la Misaada la Kiislamu Duniani, angalia, **www.lutheranworld.org/sites/default/files/lwf_and_islamic_relief_collaboration_2.pdf**

Simone Sinn, Mouhanad Khorchide, Dina El Omari (eds.), *Religious Plurality and the Public Space. Joint Christian-Muslim Theological Reflections* [Dini Nyingi na Umma.

## Vipimo vitatu vya ushiriki kwa umma


Katika kila mfano, lazima kujadili vipimo vitatu vinavyoingiliana vya ushiriki: matendo, mawazo, na mifumo. Kwa pamoja mambo haya matatu yanaweka njia iliyokamilika ya ushiriki wa kanisa sehemu za umma.

Kwanza kuna kitu, au hatua inayoonekana: matendo yanayoonekana ambapo watu wanaona kitu mara moja. Kipimo cha pili na cha tatu mara nyingi havionekani, lakini vinaweza kuwa na nguvu zaidi. Kipimo cha pili ni cha mawazo kama misimamo, fikra, masimulizi, theologia na maadili ambayo hutoa ushawishi na muongozo wa kufanya kazi. Kwa hiyo, hiki ni kipimo cha kidini-kitamaduni-kiroho. Kipimo cha tatu makubaliano ya mfumo wa kitaasisi na kimchakato vinavyoonesha nafasi ya kuingiliana katika jamii. Hii ni kipimo cha kisheria-kisiasa-kiraia. Wakati mawazo hayo yanajenga hoja kuhalalisha matendo ndani ya kanisa, mifumo inatoa uhalali na mipaka ya makubaliano toka nje. Tofauti hii inaakisi mafundisho ya wakati wote ya Kilutheri ya dola mbili zilizojadiliwa hapo juu.

Vipimo vyote vitatu vinahusiana, lakini haviko sawa. Kimoja kinaathiri kingine na kuhojiana vyenyewe kwa vyenyewe. Mawazo mara nyingi yamehamasisha na kuongoza matendo, lakini kama matendo yanabadilika, mawazo yanaweza kubadilika pia. Mielekeo hii inaweza kujionesha kati ya matendo na kanuni za kisheria.

---

Tafakari za Kitheologia za Pamoja kati ya Wakristo na Waislamu (Leipzig: Evangelische Verlagsanstalt, 2015), angalia tovuti ya **www.lutheranworld.org/sites/default/files/DTPW-Studies-201501-Religious_Plurality_in_Public_Space.pdf**




Toka mwanzo, kigezo kikubwa kwa ajili ya ushiriki wa FMKD kimekuwa kipimo kinachosaidia au kutosaidia kupunguza mateso kwa wanaoishi katika mazingira magumu. Lengo lililokusudiwa ni kufikia ushiriki wenye usawa, usalama na maana kwa kila mtu - sehemu ya haki kwa wote. Kwa njia ya ushirika wa kimataifa, matendo wanayoshirikishana makanisa, mawazo na mifumo, vinakusudia lengo hili. Hata kama kumekuwa na maendeleo katika lengo hili, bado uonevu sehemu za umma upo. Hii inahitaji kwamba ushirika, makanisa na watu binafsi wapitie juu ya juhudi zilizopita na kutafuta njia mpya za kujihusisha na umma ili kuleta mabadiliko ya maana katika jamii.

### Maswali kuhusu uhusika wa kanisa

- Ni kwa njia gani kanisa linachangia kuimarisha mifumo inayowajibika na kudadisi matatizo ya mifumo hiyo katika jamii?

- Ni kwa namna gani kanisa kwa njia ya matendo yake ya kiroho na diakonia, linawawezesha washarika wakekuwa raia wenye kushiriki katika masuala ya umma?

- Ni njia gani zenye ubunifu za ushiriki katika jamii tunaweza kuzitambua na kuzifikiria?

# ABCDE ya Uhusika wa Kanisa sehemu za Umma

## Kutathmini masuala ya umma kwa njia shirikishi

Kwa kuwa masuala mengi yanayohusu umma ni magumu na yanawahusu watendaji wengi, kuna haja ya kuyakagua kwa makini ili kuyaelewa kwa mapana yake. Hii inajumuisha kusikiliza wahanga wa jambo hilo kwa kuwahoji huko waliko. Katika mchakato huo wa utambuzi wa mahitaji na matakwa ya wadau mbalimbali kutatakiwa orodha ya mifumo kandamizi iliyojihusisha na uonevu iandaliwe kwa umakini mkubwa. Kanisa linahitaji kuwa wazi kuhusu mahusiano yake na suala linalofanyiwa kazi na kutafuta njia za kuimarisha tathmini shirikishi.

## Kujenga uhusiano wenye kuaminiana

Migogoro inazikumba jumuiya nyingi katika dunia hii. Kanisa limeitwa kutembea katika njia za amani na watendaji wengine katika jamii na kujenga mahusiano ya kuaminiana. Kanisa linatoa nafasi ya kushughulikia kwa uaminifu mipasuko iliyopo. Kanisa limeitwa kuongoza na kuhudumia michakato ya toba, uponyaji na kusameheana na kwa pamoja kutembea katika njia mpya kuelekea upatanisho kamili. Kanisa linaalika kuwa na uwajibikaji wa majukumu ya pamoja na linahusika kwa vitendo kuzishawishi asasi za kiraia, na kuwa sehemu ya mtandao wa mshikamano.

## Kupinga uonevu

Katikati ya ugumu huu, kanisa bila kuwa na mashaka yoyote linatakiwa lipaze sauti ya kinabii pale ambapo utu wa watu unahujumiwa na haki za binadamu zinakiukwa. Kuna wakati kanisa linaweza kutumia njia zilizopo kutetea wanyonge na wanaobaguliwa, na kwa wengine linahitaji kutafuta njia zingine za ziada ili kukabidiliana na uonevu. Injili ina maono ya wazi kabisa ya kubadilisha mifumo kandamizi na yenye kuleta uharibifu. Wakristo wanaitwa kushiriki katika siasa, si kwa ajili ya kupata vyeo, bali kwa ajili ya kuwawezesha wale wanaoteseka kwa uonevu. Kanisa linapigania utawala

wa sheria na utawala bora kama masharti ya juu kabisa ya kuwa mifumo muhimu kwa ajili ya kuleta haki na amani katika jamii.

## Kugundua alama za matumaini

Kanisa ni mahali ambapo linaalika watu kugundua alama za matumaini na kuunganisha na upendo wa Mungu uliokithiri kwa dunia hii. Kanisa linaaandamana na watu katika safari yao ya kiroho pale wanapolishwa Neno la Mungu na kuwa na matumaini kwa njia ya Roho wa Mungu. Kanisa linaunganishwa na juhudi zinazoangazia matumaini katika jamii kwa kufungua kurasa za fursa mpya pale ambapo watu wenyewe wanajikuta wamepotea na kukosa matumaini. Utunzaji kichungaji, juhudi za kidiakonia na kushiriki kazi za umma vinatoa njia mbadala pale ambapo watu wanajiona kuwa walikuwa wanaumia kwa sababu ya mienendo yenye uharibifu. Kushirkishana matumaini ni kipimo muhimu cha ushiriki wa kanisa kwa umma.

### Kuwezesha wahitaji

Kanisa limeahidi kuimarisha uwakala wa watu ili waweze kukuza kikamilifu uwezo wa watu wengine katika maisha yao. Injili inayo maono kwamba vikwazo vyote vinavyowazuia watu kushiriki kikamilifu katika jamii viondolewe (Luka 4:18 na kuendelea.) Kanisa lipo na watu wanaoteseka na linasikia taabu zao. Kanisa linaangalia namna ya kuwezesha wanyonge na wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa njia uwepo wa huduma za diakonia, elimu, utetezi na wakati mwingine harakati za kupinga hali hizo. Kanisa linafurahi pamoja na watu wanapopata ukombozi na uponyaji, wanapata haki na amani, na kuufurahia utu wao.

Kiambatisho

# Nafasi ya Kanisa kwa Umma - Tamko la Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani[15]

## 1. Walutheri wanakubali wito wa kushiriki katika masuala ya umma

Katika tukio la yubile ya miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa, Ushirika wa Kilutheri unaona kuwa kushiriki katika masuala ya umma ni dai lake la muhimu la kuwa Mlutheri. Ushiriki katika masuala ya umma ni jibu endelevu la kanisa kwa uhuru tulio nao katika Kristo kumpenda na kumhudumia jirani. Matengenezo ya Kanisa yalieleza bayana kuwa uhuru unatokana na wokovu kutoka neema [ya Mungu] kwa imani.

Wakati huu ambapo wajibu na mamlaka ya dini vinajadiliwa sana, tunaeleza wazi kwa nini na kwa namna gani sisi kama Walutheri tupo na kwa vitendo katika sehemu za umma. Tunapoangalia mambo ya mbeleni kama ushirika wa kimataifa, tunaitikia mwito wa kuweka mizizi ya uwepo wetu katikati ya umma.

Wakristo tumejengwa na ujumbe wa injili. Nguvu ya Mungu iokoayo inatubadilisha sisi kuishi maisha yanayotafakari habari njema ya Yesu Kristo. Katika Kristo Mungu anakumbatia udhaifu wetu, mateso na dhambi na kutuleta katika maisha mapya (Fil. 2). Ubatizo ni nanga ya maisha ya Kikristo na ushiriki wa Kikristo katika masuala ya umma. Biblia inatuita kuwa tayari kutoa majibu kwa yeyote yule anayetaka tuwajibike kwa matumaini yaliyomo ndani yetu; na tufanye hivyo kwa upole na heshima (1 Pet 3:15 na kuendelea). Ubatizo unamaanisha wito wa kuishi katika imani, matumaini na upendo (1 Kor 13:13), ni wito wa kuwa tayari kuhudumu kwa ajili ya ustawi wa wote.

Jamii za Kikristo zina kipimo cha umma, kwa kuwa zimeitwa na Mungu kuwa mawakala wa mabadiliko katika dunia (Rum 12:2). Makanisa na sharika vinaitwa kwenda mbali zaidi ya maeneo yake wanayojisikia vema na kukaa kinabii katikati ya vilio na matumaini vilivyomo ndani ya mazingira yake

[15] Tamko hili lilipitishwa na Halmashauri Kuu ya Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani katika mkutano wake Wittenberg, Ujerumani, Juni 2016.

ya kikanda na kimataifa. Kwa hiyo, makanisa yanapojitenga na masuala mapana ya jamii zao yanausaliti wito wao wa kuwa chumvi na mwanga wa ulimwengu (Mat 5:13–16).

## 2. Walutheri wanaahidi kuimarisha ushiriki wao kwa umma kama sehemu ya haki kwa wote

Tunaona sehemu ya umma kama eneo la haki kwa wote na tunakubali ahadi yetu ya kuchangia kwa vitendo kwa kwa umma. Mambo matatu yanaweka bayana tabia ya umma kama eneo la haki kwa wote: (a) kuwa na usawa katika kupata mahitaji muhimu na kushiriki mchakato wa maamuzi ya kisiasa (b) usalama, hasa kwa wanyonge; na (c) ushiriki wenye maana na mahusiano kati ya makundi yote yaliyopo kwenye jamii.

Uwezeshaji wa kijamii unachukua nafasi pale makundi ambayo kwa utamaduni uliopo yanabaguliwa na jamii, yanapopaza sauti zisikike na kudai matatizo yao yatatuliwe na umma na hivyo kuwa na uwezo wa kuchangia katika kutengeneza sera za umma na kubadili tamaduni [kandamizi].

## 3. Walutheri wanakubali wajibu na majukumu ya jumuiya za kidini

Kwa kupinga mwelekeo wa kujaribu kufanya masuala ya kidini kama mambo ya mtu binafsi na kubaki katika jumuiya zilizojifungia, tunakubali kuwa jumuiya za kidini zina wajibu katika sehemu zote za umma katika jamii. Zinachangia kwa vitendo kwenye malengo ya pamoja kwa kushirikisha maono ya kiroho na maadili, vikielezea uelewa wao juu ya jamii yenye haki na amani, na kufanya utetezi dhidi ya mifumo ya uonevu na kuwahudumia watu wenye shida.

Wajibu huu kwa umma unahusisha uwajibikaji kupanga masuala yako mwenyewe katika hali ya uwajibikaji na uwazi, ikiwa ni kwenye mambo ya kitaasisi au kwenye mambo yahusuyo mafundisho ya kitheologia. Walutheri wanauelewa makini juu ya kuwa mwanadamu ni mkosaji na mwenye dhambi, hata ndani ya kanisa lenyewe. Kwa sababu hii, kanisa haliwezi kudai kuwa liko kwenye nafasi ya juu katika masuala ya umma. Neno la injili linaleta uhai duniani na kanisa ni chombo tu ambamo injili husikiwa. Kwa hiyo, kanisa limeitwa kushiriki katika masuala ya dunia hii likiwa na nafasi ya kuhoji na kujihoji.

## 4. Walutheri wanakaza tofauti kati ya utawala wa kidunia na kiroho

Wanapodai kuwepo kwa vitendo katika umma, hivyo ni rahisi kutofautisha kati ya utawala wa kidunia na kiroho. Kwa kufuata theologia ya Kilutheri, katika utawala wa kidunia, sheria hutumika kuweka utaratibu wa maisha katika jamii ili watu wote waishi pamoja kwa amani. Katikati ya moyo wa utawala wa kiroho kinachotawala ni kushirikishana habari njema juu ya upendo wa Mungu ulio wa ndani sana kwa dunia hii. Kutangaza huruma ya Mungu ni alama muhimu ya kanisa letu na mchango wetu mkubwa kwa umma.

Walutheri wanapinga watendaji wa dini kuifanya dini kisiasa na kuifanya chombo cha siasa. Mienendo hiyo inaondoa maana na kazi ya tawala zote mbili, na kuleta uharibifu kwa jamii nzima. Jukumu la kanisa si kuwa mtawala katika umma bali kuionya dunia dhidi mtizamo au dini, Mkristo au kitu kingine vinavyoweza kugeuka kuwa itikadi inayoweza kutawala umma. Walutheri wanasisitiza umuhimu wa uhuru wa dini au imani kama njia ya kulinda nafasi ya kiroho katika maisha ya watu usiingiliwe. Walutheri wanalaani vitendo vyovyote vya kikatili, nyumbani au sehemu za umma, na lugha za kuchochea chuki zinazojiingiza kwa njia ya jina la dini.

## 5. Walutheri wanatambua kuwa maeneo ya umma ni ya kushirikiana na watu wote

Katika jamii zao, Walutheri wanaishi na watu wenye tamaduni na viapo vya dini zingine. Mazungumzo na ushrikiano ni muhimu ili kujenga ushiriki katika masuala ya umma. Kwa kuwa migogoro imezikumba jamii nyingi, kanisa linaitwa kutembea njia ya kutafuta amani na wengine na kujenga uhusiano wa kuaminiana. Kanisa linaitwa kuongoza na kuhudumia michakato ya toba, uponyaji na msamaha na kutembea kwa pamoja katika njia mpya kuelekea upatanisho. Kanisa linashiriki kwa vitendo kujenga asasi za kijamii zenye nguvu na kuwa sehemu ya mitandao ya kuleta mshikamano katika jamii.

## 6. Walutheri wanayakubali madai ya haki za binadamu kama nyenzo muhimu ya kuwezesha upatikanaji wa haki na amani

Ushuhuda wa Kikristo kwa umma unaongozwa kimsingi kwa kutathmini madhara ya maamuzi ya kisiasa kwa watu wenye shida katika jamii. Kama viumbe wa Mungu, wanadamu wote wameumbwa na utu sawa. Kwa hiyo

kanisa linaitwa kutathmini kwa upya tofauti za kitamaduni katikati na pembezoni, kati ya wenye nguvu na wanaoonewa, kati ya walio juu na chini. Katika dunia yenye tamaduni nyingi na iliyo kama kijiji, haki za binadamu zimekuwa chombo muhimu cha kuwezesha haki na amani.

## 7. Walutheri wameahidi kushughulikia mambo matano katika ushiriki wao kwa umma:

a) Kutathmini masuala ya umma kwa njia shirikishi

b) Kujenga uhusiano wenye kuaminiana

c) Kupinga uonevu

d) Kugundua alama za matumaini

e) Kuwezesha watu wenye uhitaji.

# Kikosi kazi cha kitaaluma

## Wajumbe

Askofu Mkuu Dkt. Antje Jackelén (Sweden) kama Mwenyekiti

Askofu Mstaafu Dkt. Suneel Bhanu Busi (India)

Mchg. Dkt Eva Harasta (Austria)

Dkt Eneida Jacobsen (Brazil)

Dkt Kathryn M. Lohre (Amerika)

Mchg. Lusungu Mbilinyi (Tanzania)

Dkt Jerzy Sojka (Poland)

## Wafanyakazi wa FMKD

Mchg. Dkt Simone Sinn (Ujerumani) kama mratibu

Mchg. Dkt Kenneth Mtata (Zimbabwe)

Dkt Ojot Ojulu (Ethiopia)

FUNGAMANO
LA MAKANISA
YA KILUTHERI
DUNIANI